

## DIBAJI

Shirika la Afya Duniani (WHO) ilipendekeza yakwamba mgonjwa wowote wa COVID-19 aliye thibitishwa katika maabara atengwe na kutunzwa katika Kituo cha afya. Hata hivyo, katika hali ambayo Kutenga wagonjwa wote katika vituo vya afya haiwezikani, inasisitiza kipaumbele wale wenye kadri ya matokeo mabaya zaidi. Yaani, wagonjwa wenye magonjwa makali na hali mahututi na wale wenye ugonjwa hafifu na wenye hatari ya matokeo mabaya (wenye umri wa zaidi ya miaka 60), wagonjwa wenye magonjwa wenza, kama, magonjwa sugu ya moyo na mishipa ya damu, magonjwa sugu ya kupumua, kisukari, saratani). Shirika la Afya Duniani (WHO) inapendekeza pia kutengwa na kutunzwa kwa usalama wa nyumbani kwa washukiwa wa COVID-19 wanao oneshwa dalili hafifu na kwa mikakati ya afya ya umma yanayo husika na usimamizi wa walio tangamana nawo.

Nchini Kenya kisa cha kwanza cha mgonjwa aliyedhibitishwa iliripotiwa tarehe 13 Machi 2020. Tangu hapo Kenya iliweka mikakati dhabiti kuzuia kusamba kwa ugonjwa huu. Lakini, kusambaa kwa huu ugonjwa ulipita kiwango cha 2000 mwisho wa Machi 2020. Kati ya hawo, 500 walipona kabisa na 64 walikufa. Hii inamaanisha yakwamba kulikua na visa zaidi ya 1400 wanaougua mwisho wa mda huo. Idadi hii itapoanza kukusanya na ile ya wagonjwa walio hospitalini mda huu, hali itaanza kuwa nzito kwa Mfumo wa Huduma ya Afya. Takwimu za sasa za Kenya zinaonyesha kuwa asilimia 78% ya watu walioambukizwa hawana dalili au wana dalili hafifu, na wanaweza kushughulikiwa nyumbani. Kwa ajili hii, mwongozo wa Kutengwa na kutunzwa kwa wagonjwa wa COVID-19 nyumbani imebuniwa kwa ajili ya kesi za wagonjwa zilizoongezeka hivi karibuni na kwa kukadiria kuongezaka kwa kesi za COVID-19. Hii mbinu inayoitwa, **'Jitenge System'** inalenga kupunguza shinikizo la wagonjwa wa COVID-19 hospitalini na Nchini kwa ajili ya ongezeko la maambukizi ya jamii.

Mwongozo wa kujitenga na kujitunza nyumbani kwa wagonjwa wa COVID-19 inagusia sehemu muhimu ikiwapo; ustahiki wa wagonjwa, tathmini ya uwezekano, taratibu, na mfumo wa rufaa ikiwa dalili zitaonekana kuendelea, vigezo vya kumaliza Kutengwa nyumbani, kushirikishwa kwa jamii na ufuatiliaji kati ya mengine. Marejeo ya huu mwongozo yameingwa kutoka kwa WHO na nchi zingine Lakini ikatekelezwa kulingana na hali ya Kenya.

Ninawahimiza washiriki wote wanaohusika katika utunzaji wa wagonjwa wa COVID-19 kufuata mwongozo huu na kuwafikishia walezi wote wasio rasmi wa wagonjwa hawa ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa raia wetu.



Dr. Patrick Amoth, UA

**KAIMU MKURUNGEZI MKUU**